Decemba 6, 2022

Mzazi Mlezi mpendwa:

Toka Idara ya shule za msingi na secondary (DESE), tumepokea habari njema kwamba kuna pesa zitakazo rejeshwa kwa wanafunzi kuhusiana na janga kubwa la kimataifa.

Wanafunzi waliozuwiliwa kwenda shuleni kwa sababu ya Covid-19 na hivyo hawakuweza pewa chakula ndio wanaoweza kupokea msaada huo toka Matoleo ya faida kielektroniki ya janga kuu (P-EBT) faida hizi, yaani kwa mwaka wa shule 2021-22 (SY) na kipindi cha majira ya joto (Summer) mwaka 2022. Tafadhali, chunguzeni kwa makini habari hii, kwani kumefanyika mabadiliko ya vigezo vya kustahili msaada huo.

Viongozi wa shule za Uma za Saint Louis (SLPS) wamechunga vizuri rikodi za wale waliozuiliwa na janga, itakayo saidia kurahisisha huduma hii. Tutatosha orodha ya wanafunzi na siku ngapi waliweza zuilika kwenda shuleni kwa sababu ya Covid-19. DESE itatuma orodha hiyo kwa idara ya huduma za kijamii ihusikayo na kutoa msaada kwa jamii. (FSD). Idara hiyo itaweka pesa kamili zinazotakiwa kwa kadi ya P-EBT.

**Kwa kustahili kupewa msaada toka P-EBT, kwa mwaka wa shule wa 2021-22, mtoto wako ni lazima awe:**

- Amethibitishwa na district ya shule kupewa chakula toka Programu ya Taifa ya kutowa chakula shuleni (NSLP).
- Awe mwanafunzi kwa darasa la K-12 pekee kwa mwaka wa 2021-22 (SY)
- Amekubaliwa kupewa chakula bure ao kwa kulipa semehu yake kwa mwaka wa shule wa 2021-22 (Maelezo Zaidi ni hapo chini)
- Baada ya uchunguzi kwenye orodha za shule, ameonekana kwamba alishinda nyumbani ao alifuata mafunzo kwenye mtandao kwa sababu ya Covid.

**Mtot wako hawezi pewa kitu toka P-EBT ikiwa:**

- Kwa sasa hapewi msaada wowote toka Supplemental Nutrition Assistance Program (SNAP)
- Mwafunzi hakuomba kupewa ao alikataliwa kwamba hatapewa chakula bure ao kwa kulipa sehemu yake mwakani 2021-22 (SY)

**Namna gani kuweza kupata pesa za mwaka wa 2021-2022 (SY):**
Hesabu ya siku mtoto alizoshida nyumbani bila kwenda shuleni zitatumwa kwa njia ya kipengele cha mazungumzo kwa wahusika wa msaada (tazama mfano hapo chini). Msaada utakaotolewa, utatumwa kwenye kadi uliyonayo kwa sasa na itabidi tu kuhakikisha inatumika, na hivyo kupata pesa zilizowekwa ndani.

(Ikiwa mwanafunzi wako hana kadi kwa sasa, watamtumia moja kupitia anwani iliyojazwa kwa karatasi. Ikiwa umeipoteza kadi na huna nayo tena, ita FDS kwa 855-FSD-INFO 855-373-4636.)

**Namna gani kujua hesabu ya msaada huo:**
Msaada wa pesa P-EBT itakayotoa itatokana na hesabu za siku mtoto alizobaki bila kupewa chakula bure ao kwa kulipa sehemu yake shuleni kwa sababu ya janga la COVID na hakuenda shuleni, ao akafuata majifunzo kwenye mtandao akiwa nyumbani.

(Ikiwa mwanafunzi alishinda ao akafuata majifunzo kwenye mtandao zidi ya siku tano na hasikuripotiwa kwa shule kama ni kwa sababu ya COVID imetokea, district ya shule inaweza chunguza na kuomba wazazi kutoa vitambulisho kwamba ni kwa sababu ya ugonjwa wa COVID imetokea.)

**Pandemic Electronic Benefit Transfer (P-EBT) Benefits – Page Two**

**Kulipwa kwa misaada ya Janga kwa njia ya kielektroniki (P-EBT)- Ukurasa wa pili**

**Mapashwa ili kuweza kupewa P-EBT kipindi cya majira ya joto (Summer) 2022:**
Wanafunzi waliokubaliwa kupewa chakula bure ao kwa kulipa sehemu ya pesa kwa mwaka wa shule wa 2021-22 ndio wanaokubaliwa pia kupewa msaada kwa majira ya joto (Summer) 2022. Ikiwa mtoto wako alipata chakula, kwa majira ya joto atapewa msaada kwa kulingana na hesabu za pesa za kimarekani $391. (Ona faida inavyoonekana chini).

- Ni lazima mwanafunzi awe ameorodheshwa kwa darasa la K-12 mwaka wa shule la 2021-22 ao amekubaliwa upya kupewa chakula bure ao kwa kulipa sehemu yake tangu Julai 1, 2022, hadi mwisho ya majira ya joto, ndipo atapewa msaada huo.
- Ili awe miongoni mwao watakao pewa faida ya majira ya joto (Summer), mwanafunzi ni lazima awe kwa darasa la K-12 kwa mwaka wa shule wa 2021-22.

**Kupewa bure ao kwa kulipa sehemu ya pesa inatokana na wakati mwanafunzi ame:**

- Toa ombi la kupewa chakula bure ao kwa malipo ya semehu ya pesa kwa mwaka wa shule wa 2021-22 na kuwa ameonekana kuwa anaeneza vinavyoombwa kufuatana na miongozo ya mapato kwa mwaka wa shule wa 2021-22, ao omba kupewa chakula bure ao kwa kulipa sehemu yake tangu Julai 1, 2022 hadi mwisho wa majira ya joto sawa sawa na miongozo ya mapato kwa mwaka wa shule wa 2022-23.
- Jiandikisha katika shule linalo shiriki katika uteuzi wa Utowaji wa jamii (CEP) ao Utoaji 2. Ikiwa huna uhakika kwamba shule la mtoto kuwa lina haki ya kupewa faida hiyo, unaweza wasiliana na district ya shule ambako mtoto alijifunza.
- Onekana amekuwa na haki hiyo kwa msingi wa kundi zenye kueneza mapashwa yote ikiwemo ile ya Supplemental Nutrition Assistance Program (SNAP) ao toka shirika lingine kama vile wasio na makazi ao mlezi.

Mtoto wako akiwa anaeneza mapashwa, usaidizi utapitia kadi ya P-EBT kwa jina la mtoto. Ni lazima basi, ilikupewa pesa hizo, kuhakikisha kadi inatumika.

**FAQ Kulipwa kwa faida kielektroniki toka janga la kimataifa- Ukurasa wa tatu**

**Nifanye nini ikiwa nimepoteza kadi ya mwanafunzi wangu ya P-EBT**?

Unaweza pitia kwa kipengele kifuatacho mydss.mo.gov ao kuita kwenye namba 855-373-4636.

**Nitende je? Ikiwa anwani yangu imebadilika?**

Ikiwa unafikiri kwamba mtoto wako atapewa msaada na bado anwani yenu imebadilika, unapashwa kujulisha district la shule ambako mtoto alijifunza kwa mwaka wa 2021-22 kwa kuchunguza kesi yako na kuandikia shule kuhusu mabadiliko ya anwani.

**Nimuulize nani ikiwa nina swali kuhusu kadi ya P-EBT?**

USIITE DISTRICT YA MASOMO KWA SWALI LA KADI YA P-EBT. Unaweza tumia kipengele cha mazungumzo kifuatacho mydss.mo.gov ao unaita namba 855-373-4636.

**Nimuete nani kuhusu siku ambazo mwanafunzi hakuenda shuleni**?

Ita district ambamo shule la mtoto wako linapatikana kwa mwaka wa shule wa 2021-2022.

**Nani anaweza jibu maswali kuhusu msaada wa P-EBT mwaka wa shule wa 2020-2021?**

Misaada za P-EBT toka mwaka wa shule wa 2020-21 zimetolewa na haziwezi patakana tena.

**Itakuwa je? Ikiwa shule la mwanafunzi wangu halikuhesabu siku ambazo hakuenda shule ao hawakutoa repoti za siku hizo?**

Zungumza na district ya shule ambako mtoto wako alijifunza kwa mwaka wa shule wa 2021-22 kwa kuchunguza rikodi ya siku hakuenda shuleni.

**Lini mwanafunzi wangu atapokea msaada huo?**

District ya shule la mtoto wako limekwisha tuma vinavyotakiwa kwa swali hilo la P-EBT. Ingawa hatuwezi kujua na uhakika lini kadi itakapo patikana, inawezekana wewe kupokea msaada hiyo kwa mwisho wa mwaka wa 2022.

***Ukiwa na swali kuhusu msaada wako binafsi, kama inavyoonekana hapo chini, unaweza wasiliana na Idara ya huduma za Uma za Chakula na Lishe ya Saint Louis, Althea Albert-Santiago, 314-935-5302 ao Tenecia Williams, 314-345-2308.***

***Kuna namba ya sim iliyo tayari kupokea na kujibu kwa maswali yenu- tafadhali unaweza ita 314-345-5656.***

Hapa chini ni mfano wa jedwali ya faida:

| Daraja/ Siku hakuenda | Msaada kwa siku zilizotumiwa | Hesabu ya pesa kupewa |
|---|---|---|
| Daraja 1: siku 1-5 | Siku 3 | $21.30 |
| Daraja 2: siku 6-15 | Siku 10 | $71 |
| Daraja 3: Siku 16 na zaidi | Siku 17 | $120.70 |
| Summer 2022 | Siku 55 | $391 |

Kadi za P-EBT zinatumikishwa sawa sawa na zile za EBT.Ukitaka maelezo Zaidi kuhusu kadi, unaweza enda kwa kipengele cha mazungumzo kifuatacho mydss.mo.gov/food-assistance/ebt.

Ukiwa na maulizo kuhusu namna ya kuomba, ao unahitaji msaada fulani wa chakula, ulezi wa watoto, usafiri, na/ao huduma zingine, nenda kwa Missouri Services Navigator kwenye kipengele cha mazungumzo kifuatacho mo.servicesnavigator.org